

MAUAJI KATIKA NGOME YA MASADA!



Ngome ya mwisho kuangushwa wakati wa vita ya kwanza kati ya Wayahudi na Warumi ni Masada ambayo ilipelekea kumalizika kabisa kwa vita vya kwanza vilivyodumu kwa muda wa miaka saba kuanzia mwaka 66 hadi 73BK.

Katika lugha ya Kiebrania Masada inatamkwa METSADA, inapatikana katika wilaya ya MEHOZ HA DAROM (Southern District). Ngome hii ya Masada ipo katika jabali lililojitenga ambapo juu kabisa kuna eneo tambarare mfano wa meza. Njia ya kuingia katika ngome hiyo ni nyembamba kiasi cha kutokuruhusu hata watu wawili kutembea sambamba, upana wake ultosha kwa mtu mmoja, kama ni watu wengi waliingia kwa foleni, kutokana na wembamba wa njia hiyo ya kuingia waliipa jina la NJIA YA NYOKA (snake way).

Masada iko upande wa Mashariki wa jangwa la Yudea ikitazamana na Bahari nfu (Dead Sea) iliyoko umbali wa maili kumi na mbili, kando yake ndipo kuna hifadhi inayoitwa Ein Gedi ambalo kwenye Biblia linajulikana kama Engedi.

Inasemekana kipindi kile Daudi alipokuwa akitafutwa na Mfalme Sauli aliyetaka kumuua alikuwa akajificha katika jabali la Masada na katika nyika ya Ein Gedi (1Samueli 23:29).

Kati ya mwaka 37-31 kabla ya Kristo, Mfalme Herode aliiboresha ikawa inatumika kama eneo lake la usalama.

Tangu vita ya kwanza ilipoanza mwaka 66BK ngome hiyo ilikuwa inatumiwa na Wasikarii ambaa ni tawi la Wazelote, wakati huo vikosi vya Warumi vilijaribu kupigana na ngome hiyo vikashindwa vibaya. Mwaka 70BK baada ya Hekalu pamoja na mji wa Yerusalem kuharibiwa kabisa, wapiganaji waliokuwa wakiitumia ngome hii waliendeleza



Edit with WPS Office

mashambulizi ya kuvizia wakitokea humo. Pamoja na kuwa karibu vikosi vyote vya wapiganaji wa Kiyahudi vilishaharibiwa na kuangamizwa, lakini hawa hawakuwa tayari kushindwa wala kujisalimisha!

Baada ya kumaliza majukumu yake, jemedari Tito alirudi Roma, akamteua LUCIUS FLAVIUS SILVA kuwa liwali na kiongozi wa mapigano. Akiwa na kikosi cha wapiganaji wa kirumi kilicho julikana kama LEGIO X FRENTENSIS kilichokadiriwa kuwa na wapiganaji wasiopungua 8,000 pamoja na Wayahudi 7,000 ambaao walikuwa ni mateka wa kivita, wakifanya jumla ya wapiganaji 15,000 mwishoni mwa mwaka 72BK walianza kuihusuru ngome ya Masada.

Kwa wakati huo ngomeni walikuwa wakiishi wapiganaji wa kikosi cha Wasikarii pamoja na familia zao pamoja na baadhi ya Wayahudi walonusurika ulipoharibiwa mji wa Yerusalem, jumla yao wakiwa watu 967. Idadi hiyo ilijumuisha watoto, wazee, wanawake na wapiganaji. Inaweze kana idadi ya wapiganaji ilikuwa ni nusu ya idadi hiyo. Ni wazi kuwa watu mia tano wasingeweza kutoka kwenda kupigana na jeshi lilowazingira lililokuwa na ukubwa mara thelathini kuwazidi.

Josephus Flavius, mwanahistoria aliyerekodi tukio hili, anadai Eleazar Ben Yair kamanda wa wapiganaji waliokuwemo humo ngomeni, alikuwa anawatia moyo wenzake kuwa masalia ya wapiganaji waliokuwepo kwenye viunga vya Yudea wangekuja kuwasaidia lakini haukutokea msaada wowote!

Baada ya kuizingira ngome hiyo ya Masada kwa muda wa miezi minne, tarehe 16, Aprili, 73BK Lucius Flavius Silva aliwaamuru wapiganaji wake waingie ndani ya ngome wakiwa wamejihami kwa silaha nzito. Tofauti na matarajio, hawakukutana na upinzani wowote, hawakukuta mtu yeote aliyekuwa hai, walikuta maiti 960 zilizokuwa zimeshaanza kuharibika, katika kukagua zaidi walikutwa wanawake wawili pamoja na watoto watano wakiwa hai!

Kumbe baada ya kuona jinsi jeshi la Warumi lilivyokuwa kubwa sana na jinsi ambavyo masalia ya Wayahudi wenzao jinsi ambavyo hawaji kuwasaidia, waliona ni bora wauane wenyewe kuliko kuuliwa au kuchukuliwa mateka na Warumi!

Katika imani ya Kiyahudi ni dhambi mtu kujiua, katika kuiepuka hiyo hatia, Eleazar Ben Yair alitenga kikosi cha kuua wenzao, walipomaliza kazi walijopewa akateuliwa mmoja kati yao kuua wenzake, kisha mwishowe naye akajimalizia, hatia ya kujiua ikawa juu yake peke yake. Watu saba walonusurika walijificha katika mojawapo ya mashimo mle jabalini.

Kabla ya kuuana wenyewe waliteketeza mali zao zote zikiwemo silaha, lakini akiba yote ya chakula walichokuwa nacho walikiweka mahali pa wazi ili isije ikadhaniwa kama wamejiua kwa kuwa wamekosa chakula!

Mmoja wa watu walonusurika alisimulia hotuba ya mwisho iliyo tolewa na kiongozi wao



Edit with WPS Office

Eleazar Ben Yair, baadhi ya maneno yaliyonukuliwa na Josephus Flavius ni haya:

"Tangu mwanzo sisi tulishaamua kuwa kamwe hatutakuwa watumwa wa Warumi, wala hatutamtumikia mwanadamu yeyote isipokuwa Mungu pekee, ambaye peke yake ni wa kweli na wa haki Bwana wa wanadamu wote, wakati umefika sasa ambapo inatupasa kudhihirisha uamuzi wetu huu katika matendo .. Sisi tulikuwa wa kwanza kuasi dhidi ya udhalimu wa Warumi, na sisi ni wa mwisho kupigana nao; na naheshimu kama hayo ndio mapenzi ya Mungu aliyotuamulia, kwamba bado tuna uwezo wa kufa kwa ujasiri, na katika hali ya uhuru." -Eleazar Ben Yair-

Ni Mwisraeli namba tatu

Alex E. Bubelwa

0782910000

0758298888



Edit with WPS Office